# THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

**KENYA JUNIOR SCHOOL EDUCATION ASSESSMENT**

**KJSEA**
**902/1**
**KISWAHILI LUGHA**
**Karatasi ya 1**
**SAMPLE PAPER**
**Januari 2025**
**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. Umepewa **kijitabu** hiki na **karatasi ya majibu.** Kijitabu hiki kina maswali **50.**
2. Jibu maswali **yote** kwenye **karatasi ya majibu** uliyopewa kujibia maswali na wala **sio** katika kijitabu hiki.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida, aina ya HB.
4. Hakikisha kuwa **karatasi ya majibu** uliyopewa ina:
   **NAMBARI YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
   **JINA LA SOMO**
5. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
6. Kwa kila swali, **1 – 50** umepewa majibu manne, A, B, C, D. Chagua **jibu sahihi.**
7. Kwenye karatasi ya majibu, onyesha jibu sahihi kwa **kuchora kistari** katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa jibu sahihi.

   **Mfano:**
   **Katika kijitabu cha maswali:**

   **25.** Orodha ifuatayo ni ya majina ya vitu vinavyopatikana katika mazingira yako. Ni jibu lipi lenye vitu vinavyotajwa na nomino za ngeli ya I-ZI?
   A. kucha, sahani
   B. kuta, ngoma
   C. nyuta, kamba
   D. pamba, taa

   Jibu sahihi ni '**D'.**
   **Katika karatasi ya majibu**, palipo na visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **25**, chora kistari ndani ya kisanduku chenye herufi **D**.

   **25.** [A] [B] [C] **[D]**

8. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
9. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu,** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 13 zilizopigwa chapa.**
**Hakikisha kuwa kurasa zote zipo na maswali yapo ipasavyo.**

*© 2025, The Kenya National Examinations Council*

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **1** hadi la **6.***

Watu wengi hushangaa jinsi ulimwengu unavyobadilika kwa mwendo wa kasi. Maendeleo yanazidi kushuhudiwa katika sekta za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, ni dhahiri kuwa maendeleo haya yameiletea jamii manufaa na madhara.

Sekta ya kijamii imekumbwa na mabadiliko si haba. Hapo awali, jamii nyingi ziliienzi na kuikumbatia mienendo ifaayo. Mtoto aliyeonyesha dalili za kupotoka, kwa mfano, alikashifiwa vikali sio tu na wazazi au walezi wake bali na jamii nzima. Mtoto alikuwa mali ya jamii. Kwa sababu hiyo, jamii ilimwelekeza ilivyostahili ikifahamu kuwa, mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Katu jamii **haikumdekeza** mtoto, bali ilimrudi aliyekosa papo hapo.

Inasikitisha kuona jinsi ambavyo mambo yamebadilika kwa upande wa mavazi. Yamekuwa mazoea kwa baadhi ya waja kuvalia mavazi yanayowaacha nusu uchi! Isitoshe, wengine wao hujipiga picha na kuzisambaza kwenye mitandao bila soni. La ajabu ni kwamba, wanaofanya hivyo ni wakubwa kwa wadogo, wake kwa waume.

Kwa upande mwingine, baadhi ya vijana huwavunjia heshima wakubwa wao. Utawapata katika matwana wameziba masikio yao kwa vidude hata wanapoombwa kiti na mzee hawasikii. Nayo lugha wanayoitumia kuwasiliana na wazee hawa imekosa adabu. Sikwambii vituko wanavyovifanya hadharani. Ajabu! Wanaenda kinyume cha mila na desturi za jamii zao na kusahau kuwa mwacha mila ni mtumwa.

Ukweli ni kwamba, uadilifu ni muhimu kwa mtu yeyote. Maadili hayafai kupuuzwa eti kwa sababu ya maendeleo. Watu wote wanafaa kuwa na mienendo inayokubalika katika jamii. Maendeleo yawe njia ya kuendeleza jamii bali si ya kuididimiza.

**1.** Kulingana na kifungu, ni kweli kuwa:

A. Maendeleo yoyote huwa na faida na hasara.
B. Mabadiliko ulimwenguni hupendwa na watu wengi.
C. Kuwepo kwa sekta mbalimbali huathiri maendeleo.
D. Uchumi unabadilika haraka sana ulimwenguni.

**2.** Kwa mujibu wa kifungu, malezi ya mtoto yalihusisha jamii nzima kwani:

A. Mtoto alisifiwa na jamii yake kama ilivyohitajika.
B. Mtoto aliyefanya makosa alishtakiwa na wazazi na walezi.
C. Wanajamii wengi waliheshimu na kuthamini maadili.
D. Wanajamii wote walishiriki kurekebisha tabia za watoto.

**3.** Kwa kurejelea aya ya **tatu**, chagua jibu linaloonyesha jinsi jamii ilivyobadilika.

A. Watu wengine wanavaa mavazi yasiyowasitiri vyema.
B. Siku hizi watu hupenda kupiga picha.
C. Mitandao inawavutia watu ambao hawana haya.
D. Jamii hushangazwa na mitindo mbalimbali ya mavazi.

**4.** Bainisha jinsi vijana wanavyokosa nidhamu kulingana na aya ya **nne**.

A. Husikiliza muziki wanaposafiri.
B. Wanawadharau wazee.
C. Wanatumia lugha isiyoeleweka.
D. Hupuuza jamii.

**5.** Mambo yafuatayo yanaweza kutendeka jamii ikisahau utamaduni wake **isipokuwa:**

A. Uhusiano kati ya vijana na wazee utazorota.
B. Amani itakosekana katika jamii.
C. Wanajamii watakuwa kama wafungwa.
D. Vijana wengi watajiendeleza kiuchumi.

**6.** Neno, **haikumdekeza** limetumiwa katika kifungu. *Chagua kisawe cha neno hilo.*

A. haikumridhisha
B. haikumhimiza
C. haikumbembeleza
D. haikumfurahisha

**Geuza ukurasa**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **7** hadi la **12.***

Zamani, Paka na Panya walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Waliishi pamoja na kufanya shughuli nyingi kwa ushirikiano. Waliwinda, wakapika, wakaosha vyombo na hata kufua nguo zao pamoja. Wakati mwingine, walifanya kazi zao kwa zamu.

Siku moja, Paka na Panya walipata mwaliko wa kuhudhuria harusi kati ya Beberu na Mtamba. Walifurahi kama kibogoyo aliyeota meno. Kila mmoja wao aliuona mwaliko huo kuwa fursa nzuri ya kujifurahisha. Panya alitamani kula vyakula vitamu harusini.

Paka naye, alipanga kuonyesha madaha yake. Kawaida yake, Paka alijivunia ngozi yake ya kupendeza yenye madoadoa meupe na meusi. Wote wawili walianza kujiandaa kwa minajili ya siku hiyo adimu na muhimu. Walijishonea nguo za vitenge zilizopendeza mno.

Kabla ya siku ya sherehe, Paka na Panya walivaa marinda yao ili kuhakikisha yalikuwa sawa. Panya alimwangalia Paka akagundua kuwa rinda lake lilikuwa maridadi zaidi**. Alimwonea gere**. Usiku huo, Panya aliamka usiku wa manane na kunyatanyata hadi lilipokuwa rinda la Paka. Aliliumauma likararuka raruraru kisha akarudi kulala.

Siku ya siku ilipofika, Paka na Panya waliamka alfajiri mbichi kujitayarisha. Walioga kisha wakaelekea kuvaa marinda yao. Salaale! Rinda la Paka lilikuwa tambara lisilotamanika. Paka hakuamini macho yake. Machozi yalimtiririka njia mbilimbili. Panya alijifanya kumhurumia Paka. Hata hivyo, Paka alijua kuwa tendo hilo la kinyama halikufanywa na mwingine ila Panya. Paka alipandwa na mori akataka kumvamia Panya. Panya alipoona hayo, alimwomba mwenzake amsamehe. Paka alimsamehe lakini moyoni alijiambia kuwa, kweli kikulacho ki nguoni mwako. Tangu siku hiyo, urafiki wa Paka na Panya uliingia doa.

**7.** *Chagua jibu linaloonyesha kuwa Paka na Panya walikuwa na uhusiano mwema.*

A. Walisaidiana kufanya mambo mengi.
B. Walikuwa majirani ambao walitegemeana.
C. Waliwinda baada ya kupikiana chakula chao.
D. Walifanya kazi kwa wakati ufaao.

**8.** Kwa mujibu wa kifungu, Paka na Panya walikuwa na hamu ya kuhudhuria harusi kwani

A. wangepata nafasi ya kuwaona maarusi.
B. wangeona nguo mpya za wenzao.
C. wangesafiri pamoja kama walivyozoea.
D. wangeburudika katika karamu hiyo.

**9.** Kifungu kimebainisha kuwa Paka ni

A. mwenye kiburi, mnyonge
B. mwenye kuwajibika, mpole
C. mwenye bidii, mtukutu
D. mwenye kupuuza, mtiifu

**10.** Unafikiri Panya alifanya nini baada ya Paka kumsamehe?

A. Aliwaomba maarusi waahirishe harusi.
B. Alificha nguo ambayo alikuwa ameharibu.
C. Aliahidi kuwa rafiki mwaminifu.
D. Alipika vyakula kama vya harusi nyumbani.

**11.** Matukio yafuatayo yalitokea katika kifungu.
(i) kuoga
(ii) nguo kuraruliwa
(iii) kuvaa marinda
(iv) kushona nguo

*Chagua mfuatano sahihi wa matukio hayo.*

A. (iv) (ii) (iii) (i)
B. (i) (iii) (ii) (iv)
C. (iv) (iii) (ii) (i)
D. (i) (ii) (iii) (iv)

**12.** Nahau, **alimwonea gere** imetumiwa katika kifungu. Maana yake ni

A. alikuwa na hasira kwake.
B. alikuwa na wivu kwake.
C. alimpangia njama.
D. alimtendea ukatili.

**Geuza ukurasa**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **13** hadi la **17.***

Miaka ya nyuma, jamii nyingi humu nchini zilijivunia kuwa na watu waliomiliki nguvu za kiajabuajabu. Watu hawa waliokuwa na nguvu zisizo za kawaida, waliogopwa na kuheshimiwa. Walichukuliwa kama kitambulisho cha jamii zao.

Katika jamii ya Akamba, hadithi husimuliwa kumhusu nabii wa kike aliyeitwa Syokimau. Syokimau aliishi katika karne ya kumi na tisa kwenye milima ya Iveti, karibu na mji wa Machakos. Inasemekana kuwa, licha ya kuwa nabii, Syokimau alikuwa mganga mahiri. Alikuwa na uwezo wa kutabiri matukio ya baadaaye na kutibu magonjwa mbalimbali.

Ubashiri wa Syokimau uligonga ndipo; kila alichotabiri kilitukia. Alitabiri kuhusu uvamizi kutoka kwa jamii jirani mathalan Agikuyu na Maasai. Uvamizi huo ulipotokea uliwapata wapiganaji wa jamii yake wakiwa wamejiandaa. Aliona joka refu lililokuwa likitema moto pamoja na moshi. Joka hilo liliwashusha watu waliokuwa na ngozi iliyofanana na nyama. Haya **yalitimia** wakati ambapo wazungu walikuja na kujenga mtambo wa reli. Syokimau alibashiri kuhusu kuzuka kwa kizazi cha kushangaza ambacho kingevunja miiko. Kizazi cha sasa kina mitindo isiyoeleweka katika mavazi yao na lugha wanayotumia.

Syokimau aliagua ndwele mbalimbali zilizowasumbua watu wa jamii yake. Baadhi ya ndwele hizo zilishukiwa kuwa za kishirikina. Kipawa hiki kilimfanya Syokimau kuheshimiwa na watu wa jamii yake.

Kifo cha Syokimau ni kitendawili. Kuna madai kuwa alifariki na kufufuka mara mbili kabla ya kuaga dunia kabisa mara ya tatu. Inaaminika kuwa eneo la sasa la Syokimau limepewa jina hilo kutokana na shujaa huyo. Hali kadhalika, mnara umejengwa kwa heshima yake katika kituo cha Reli cha Syokimau.

**13.** Kulingana na aya ya **kwanza,** wanajamii

A. walidumisha heshima ya eneo lao.
B. waliwaamini viongozi wa jamii zao.
C. walijulikana kutokana na asili yao.
D. walifurahia uwezo wa mashujaa wao.

**14.** Syokimau alitabiri mambo mbalimbali. *Chagua jibu ambalo **halionyeshi** utabiri wa Syokimau.*

A. Kuvumbuliwa kwa gari moshi nchini.
B. Kupuuzwa kwa mila na desturi.
C. Kushinda maadui katika jamii.
D. Kuja kwa wageni kutoka mbali.

**15.** *Chagua jibu linaloonyesha sifa ya jamii ya Akamba katika kifungu hiki.*

A. Wanawathamini viongozi wao.
B. Wanajua mbinu nyingi za kupigana.
C. Walikumbwa na magonjwa ya kishirikina.
D. Walificha matendo ya mashujaa.

**16.** Je, unafikiri jamii ya Akamba ilifanya nini baada ya kifo cha Syokimau?

A. Walipata shujaa kutoka jamii nyingine.
B. Walitafuta namna ya kujitibu kila walipougua.
C. Waliogopa kupigana ili wasije wakashindwa.
D. Walianzisha utamaduni mpya na kushauriana.

**17.** Maana ya neno **yalitimia** kulingana na kifungu ni

A. yalienezwa.
B. yalikumbukwa.
C. yalisifika.
D. yalitendeka.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la **18** hadi la **20**.*

Bwana Muka anaishi katika mtaa wa Tusonge. Bwana Muka hufanya biashara ya kuuza mapambo. Ana duka kubwa la jumla katika mtaa huu. Wateja wake wakuu ni Taira, Karo, Gidioni na Andere. Wateja hawa hununua mapambo na kwenda kuyauza rejareja sokoni. Kila mmoja wa wateja hawa ana siku ambapo hununua mapambo ya aina fulani. Tazama jedwali lifuatalo:

| **Siku** / **Mteja** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
|---|---|---|---|---|---|
| **Taira** | vipuli | bangili | mikufu | pete | taji |
| **Karo** | bangili | bangili | pete | mikufu | pete |
| **Gidioni** | mikufu | pete | pete | mikufu | taji |
| **Andere** | taji | bangili | bangili | bangili | taji |

**18.** *Chagua jibu lenye jina la mteja ambaye hununua mapambo ya aina mbili* ***pekee.***

A. Andere
B. Taira
C. Karo
D. Gidioni

**Geuza ukurasa**

**19.** Watu wa mtaa wa Tusonge wanapenda pambo gani zaidi?

A. mikufu
B. pete
C. taji
D. bangili

**20.** *Chagua jibu lenye siku ambayo kila mteja wa Bwana Muka hununua pambo linalotofautiana na la wenzake.*

A. Jumanne
B. Ijumaa
C. Alhamisi
D. Jumamosi

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la* ***21*** *hadi la* ***25.***

*(Ni asubuhi. Kweyu amesimama kando ya barabara kuu karibu na kivukomilia. Kweyu ameshika mkongojo ambao anaugotagota chini mara kwa mara. Musimba anatembea akielekea upande alipo Kweyu. Anamfikia.)*

| | |
|---|---|
| Musimba: | Ndugu, habari gani? |
| Kweyu: | *(Akiangalia upande ilikotokea sauti.)* _21__mwenzangu. |
| Musimba: | *(Kwa upole.)* Nimekuona hapa kwa muda! Nikusaidie vipi ndugu yangu? |
| Kweyu: | *(Akitabasamu.)* Kweli nimekuwa hapa kwa muda. Ninaomba unisaide kuvuka barabara hii. Magari yanapita kwa kasi. |
| Musimba: | Naam! Magari kwenye barabara kuu huendeshwa haraka sana. |
| Kweyu: | Ukinisaidia, nitashukuru sana. *(Kimya.)* Wewe unaitwa nani? |
| Musimba: | Mimi ninaitwa Musimba. Wewe unaitwa nani na unaelekea wapi? |
| Kweyu: | Mimi ninaitwa Kweyu. Ninaelekea hospitali ya macho ya Inuajamii. Miaka miwili iliyopita, nilianza kuwa na matatizo ya macho. Baada ya muda mfupi, jicho langu moja lilipoteza uwezo wa kuona. Leo nina miadi na daktari hospitalini humo. |
| Musimba: | *(Akionyesha kusikitika.)* Usitie shaka. Nitakusaidia kuivuka barabara. Tutatumia kivukomilia kile. Ninaamini kwamba Mola atakuponya. _25__ *(Akimshika mkono.)* Twende. *(Wanavuka salama.)* |

**21.** Chagua jibu sahihi kukamilisha nafasi ya **21** iliyoachwa kwenye kifungu.

A. Chewa
B. Aheri
C. Sijambo
D. Njema

**22.** Ili mazungumzo yafanikiwe, wazungumzaji wanapaswa kujenga uhusiano mwema. Chagua jibu linaloonyesha kuwa Kweyu na Musimba walijenga uhusiano mwema.

A. Walifahamishana majina yao walipokutana.
B. Walikubaliana kuwa magari yanaendeshwa kwa kasi.
C. Walitumia kivukomilia kuvuka barabara.
D. Waliamini kwamba tatizo lao lingepata suluhisho.

**23.** Vipengele vifuatavyo vya Kusikiliza na Kuzungumza vimebainika katika mazungumzo haya **isipokuwa**

A. kutumia ishara wakati wa mazungumzo.
B. kuzungumza kwa zamu.
C. kuzungumza mwingine akizungumza.
D. kuuliza na kujibu maswali.

**24.** Kweyu alimsimulia Musimba chanzo cha hali yake ya kutoweza kuona. Unadhani Musimba angetumia neno gani kuonyesha hisia zake kuhusu hali hiyo?

A. Kumbe!
B. Maskini!
C. Hamadi!
D. Kefule!

**25.** Chagua nahau inayofaa kujaza nafasi ya **25** katika kifungu.

A. Jipe moyo.
B. Fanya haki.
C. Pata fursa.
D. Shika usukani.

**Geuza ukurasa**

*Kifungu kifuatacho kina nafasi **26** hadi **35**. Umepewa majibu* **manne** *hapo. Chagua jibu lifaalo* ***zaidi*** kujaza nafasi.

Usalama ni hali ya kuwa na amani. __26__ hakuna amani bila shaka kuna fujo. Ni muhimu __27 usalama __28__shuleni. Je __29__tunapaswa kufanya nini ili tuwe salama? Inatubidi __30__ kuhusiana na watu tusiowafahamu. Kwa njia hii tutazuia hatari kama vile kutekwa nyara. Jambo lingine ni kujihadhari na matumizi ya vifaa hatari. Tukumbuke kukausha maji yote kwenye sakafu __31__ili tusiteleze na kuanguka. Ni __32__kushiriki michezo __33__. __34__ tunafaa kushirikiana kudumisha usalama kwani __35__.

**26.** A. Lau B. Ikiwa C. Ilhali D. Pengine

**27.** A. kujihakikishia B. kunihakikishia C. kukuhakikishia D. kumhakikishia

**28.** A. tumekuwa B. tungekuwa C. tunapokuwa D. tulipokuwa

**29.** A. , B. / C. : D. !

**30.** A. tuepushe B. tuepukie C. tuepukiwe D. tuepuke

**31.** A. tukipiga hema B. tukipiga deki C. tukipiga soga D. tukipiga mbizi

**32.** A. wema B. mwema C. njema D. vyema

**33.** A. zinazofaa B. wanayofaa C. inayofaa D. yanayofaa

**34.** A. Sote B. Vyote C. Nyote D. Yote

**35.** A. baada ya dhiki faraja. B. mkono mmoja haulei mwana.
C. mtaka cha mvunguni sharti ainame D. kila mwamba ngoma huvutia kwake

*Kutoka swali la **36** hadi la **50** chagua jibu sahihi.*

**36.** Neno, **huruma** katika sentensi, **Matu alimwonea huruma,** ni nomino dhahania.
*Chagua jibu linaloonyesha aina za nomino zilizopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:*

<u>Baraza</u> la wazee liliamua <u>kesi</u> hiyo kwa wakati ufaao.

A. pekee, wingi
B. kawaida, pekee
C. wingi, makundi
D. makundi, kawaida

**37.** Ni sentensi gani iliyo katika hali ya kuendelea?

A. Mashabiki watakuwa wakishangilia wakati huo.
B. Nyumba nzuri zimejengwa huku mashambani.
C. Mashairi yakikaririwa kwa ustadi, huvutia wengi.
D. Nyota humetameta angani nyakati za usiku.

**38.** Neno **wangali** katika sentensi: Wanariadha wangali uwanjani, ni kitenzi kishirikishi. *Chagua sentensi nyingine yenye kitenzi kishirikishi.*

A. Benja amekuwa akicheza soka tangu mwaka jana.
B. Asha anaelewa kuwa matunda huimarisha afya.
C. Katana amekuwa mtangazaji hodari nchini humu.
D. Tito alifaulu kwa kuwa alishirikiana na wenzake.

**39.** Nomino, **cheti** iko katika ngeli ya KI-VI. Nomino, **mpini** iko katika ngeli gani?

A. U-YA
B. U-I
C. I-ZI
D. I-I

**40.** *Chagua neno sahihi kujaza nafasi katika jedwali lifuatalo. Fuata mfano.*

| | |
|---|---|
| ndefu | fupi |
| imara | __________________ |

A. legevu
B. dogo
C. rahisi
D. mbaya

**41.** Ukanusho wa sentensi, **Amewekeza fedha zake kwenye mradi huo** ni:

A. Hatawekeza fedha zake kwenye mradi huo.
B. Hakuwekeza fedha zake kwenye mradi huo.
C. Hangewekeza fedha zake kwenye mradi huo.
D. Hajawekeza fedha zake kwenye mradi huo.

**Geuza ukurasa**

**42.** *Chagua jibu lenye kiambishi kinachofaa kujaza nafasi katika sentensi ifuatayo.*
Zulia ___ lifumwa vizuri.

A. ki
B. zi
C. li
D. vi

**43.** *Chagua usemi halisi wa:*
Kefa alimwahidi Juma kwamba angemsaidia kukuza kipawa chake cha uchoraji.

A. "Atanisaidia kukuza kipawa chako cha uchoraji," Kefa alimwahidi Juma.
B. "Nitakusaidia kukuza kipawa chako cha uchoraji," Kefa alimwahidi Juma.
C. "Atakusaidia kukuza kipawa chako cha uchoraji, " Kefa alimwahidi Juma.
D. "Nitamsaidia kukuza kipawa chako cha uchoraji," Kefa alimwahidi Juma.

**44.** Mwenzako amekuomba umwonyeshe sentensi yenye kivumishi cha idadi. Utachagua sentensi ipi?

A. Insha chache zilizoandikwa ziliwavutia.
B. Matunda yao yameiva haraka.
C. Viatu vile vimetengenezwa kwa ngozi.
D. Nguo chafu zitaoshwa kesho.

**45.** *Chagua jibu lenye sentensi iliyoakifishwa ipasavyo.*

A. Huree, tumeshinda mechi hiyo.
B. Huree? Tumeshinda mechi hiyo.
C. Huree: tumeshinda mechi hiyo.
D. Huree! Tumeshinda mechi hiyo.

**46.** Sentensi, **Kanga alimpikia nyanya yake uji,** inamaanisha Kanga alipika uji ili nyanya yake anywe. *Chagua jibu lenye maana **nyingine** ya sentensi hiyo.*

A. Kanga alipika uji akiwa kwa nyanya yake.
B. Kanga alipika uji kwa kuelekezwa na nyanya yake.
C. Kanga alipika uji kwa niaba ya nyanya yake.
D. Kanga alipika uji baada ya nyanya yake.

**47.** Sentensi zifuatazo zimetumia mbinu mbalimbali za lugha. *Chagua sentensi ambayo imetumia sitiari.*

A. Sidai alitia fora kwenye tamasha za muziki mwezi jana.
B. Wambu ni taa ya jamii nzima baada ya ushindi huo.
C. Kibicho alirudi kwao akiwa mzima kama kigongo.
D. Tongani anafahamu kwamba mvumilivu hula mbivu.

**48.** *Chagua jibu lenye maana ya maneno yafuatayo: ghali, kali.*

A. thamani ya juu, yenye uchachu.
B. yenye umuhimu, ladha ya kuwasha.
C. faida ya kitu, yenye uchungu.
D. yenye ubora, kiwango cha juu.

**49.** Ni sentensi ipi iliyo katika hali ya ukubwa?
A. Jokofu hilo liliuzwa sokoni jana.
B. Jino lililokuwa likiuma lilitibiwa.
C. Joto hilo lilikuwa kali sana.
D. Jipira limepigwa kwa ustadi mkuu.

**50.** Mwenzako anapuuza ushauri anaopewa kuhusu mienendo yake mibaya. *Chagua methali utakayotumia kumwonya.*

A. Ukiujua huu, huu huujui.
B. Mwana wa mhunzi asiposana huvuvia.
C. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
D. Sikio la kufa halisikii dawa.

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**